Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**MASUDI ALISEMA SELEMANI**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 042/2019**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**5 JUNI 2026**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, 5 Juni 2026:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa Hukumu katika kesi ya *Masudi Said Selemani dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Masudi Selemani* (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Lilungu mkoani Mtwara, baada ya kukutwa na hatia ya mauaji na akahukumiwa kifo kwa kunyongwa. Mleta Maombi alidai kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki yake ya kuishi, haki ya utu wa asili, haki ya kuwakilishwa na wakili amtakaye, haki ya kuhukumiwa ndani ya muda unaofaa na haki ya kusikilizwa, zinazolindwa kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1)(c), 7(1)(d) na 7(1) vya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) mtawalia kuhusiana na kesi katika mahakama za kitaifa.

Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), ina mamlaka ya kutoa hukumu moja kwa moja, ama kwa kuombwa na Mleta Maombi au kwa hiari yake, ikiwa masharti yaliyomo katika Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama yalitimizwa. Katika suala hili, hukumu ya moja kwa moja ilitolewa kwa uamuzi wa Mahakama, kwani Mahakama iliridhika kwamba Mjibu Maombi alikuwa

amepewa hati zote zinazohusiana na kesi; na kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekosea kwa kushindwa kuwasilisha Majibu yake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), Mahakama iliona kwamba ilipaswa kwanza kuamua endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Maombi haya kuwasilishwa, mnamo tarehe 19 Oktoba 2019.

Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka halisi kwa sababu Mleta Maombi alikuwa amedai kuna ukiukaji wa haki zake, zinazolindwa kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1)(c), 7(1)(d) na 7(1) vya Mkataba. Aidha, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, ambacho maudhui yake yamerudiwa katika Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 50(2) cha Kanuni za Mahakama, Maombi haya yalikuwa yametimiza masharti ya ukubalifu yafuatayo: Mleta Maombi alikuwa ametambuliwa kwa kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi haya yalitimiza Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha,

Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Maombi haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibaini kuwa Mleta Maombi alikuwa amekata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa, ambacho ni chombo cha juu cha mahakama ya Mjibu Maombi, uamuzi wa Mahakama Kuu ukimtia hatiani kwa mauaji. Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wake tarehe 22 Novemba 2014, ikitupilia mbali rufaa ya Mleta Maombi. Kwa hivyo, Mleta Maombi alikuwa amekamilisha taratibu za ndani kwa kuzingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama iliona tena kwamba Maombi ambayo yaliwasilishwa miaka minne, miezi minane na siku nane baada ya Mahakama ya Rufaa kutoa uamuzi wake tarehe 22 Novemba 2014, yaliwasilishwa ndani ya muda unaofaa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Hii ni kwa sababu Mleta Maombi alifungwa na kutengwa na watu, alikuwa na uwezo mdogo wa kutembea na uwezo mdogo wa kupata habari. Mahakama pia ilijiridhisha kwamba Maombi haya hayakuibua madai ambayo tayari yalisuluhishwa mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia iliangalia endapo Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki za Mleta Maombi kwa mujibu wa Vifungu vya 4, 5, 7(1) (c), 7 (1) (d) na 7(1), kwa mwenendo wake katika tathmini ya ushahidi na kumhukumu kifo Mleta Maombi.

Mleta Maombi aliwasilisha kwamba hukumu yake ilikiuka haki yake ya kuishi chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, akidai kwamba ushahidi wa mashtaka haukutosha na kwamba hakukusudia kufanya mauaji. Mahakama ilirejelea kwamba Kifungu cha 4 kinakataza kuondolewa uhai kiholela, ambacho kinahitaji kutathmini endapo hukumu hiyo ni halali na imetolewa na mahakama yenye uwezo kulingana na mchakato unaostahili. Madai ya Mleta Maombi yanahusiana tu na mchakato unaostahili. Katika

suala hili, Mahakama ilisisitiza kwamba haitathmini tena ushahidi ambao tayari umeangaliwa na mahakama za kitaifa. Baada ya kuangalia kumbukumbu, haikuona kosa dhahiri katika tathmini ya ushahidi wa shahidi au katika hukumu ya Mleta Maombi ambalo lingesaidia kubaini kwamba haki za Mleta Maombi zilikiukwa kama inavyodaiwa. Hata hivyo, Mahakama iliona kwamba kutolewa kwa hukumu ya lazima ya kifo, bila uwezekano wa kutumia busara ya mahakama, kunakiuka mchakato unaostahili. Kwa hivyo, ni kuondolewa uhai kiholela na kukiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba.

Mleta Maombi pia alidai kuwa kutolewa kwa hukumu ya kifo kwa kunyongwa, pamoja na kuwekwa kwake kizuizini kwa muda mrefu kwenye jela ya wanaosubiri kifo, kulimweka katika mazingira yasiyo ya kibinadamu ya kukosa tumaini la kuishi, kwa kukiuka haki yake ya utu wa asili. Mahakama iliona kwamba muda mrefu akiwa kwenye jela la wanaosubiri kifo na njia ya kuuawa kwa kunyongwa ni kudhalilisha utu wa binadamu.

Kuhusiana na madai ya ukiukaji wa haki ya kuwakilishwa na wakili wa chaguo lake, Mahakama haikupata ushahidi wowote kwamba Mjibu Maombi alizuia upatikanaji wa wakili kwa ajili ya Mleta Maombi, kuzuia mashauri, au kunyimwa muda na nyenzo za kutosha kwa ajili ya maandalizi ya utetezi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba haki ya Mleta Maombi ya kuwakilishwa na wakili wa chaguo lake haikuwa imekiukwa.

Mahakama iliona kwamba kipindi cha miaka miwili na miezi saba kati ya kukamatwa kwa Mleta Maombi na kuanza kwa kesi haukuwa muda usiofaa. Ilibainisha kuwa michakato ya kabla ya kesi ikiwa ni pamoja na uchunguzi, kurekodi taarifa za mashahidi, na kuwasilisha faili la kesi kwa Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma, ni muhimu na huchukua muda mwingi. Mahakama iliendelea kuona kwamba muda unaotumika kwenye michakato hiyo unaweza kutofautiana kulingana na mzigo wa kazi na ratiba ya mamlaka husika za mahakama.

Kwa madai kwamba Mleta Maombi hakunufaika na usaidizi wa mkalimani kwamba aliruhusiwa kuwaita mashahidi katika utetezi wake, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi aliwakilishwa na wakili na hakuomba msaada wa mkalimani katika hatua yoyote ya kusikiliza kesi. Ilibainisha pia kwamba Mleta Maombi alipinga kikamilifu ushahidi wa upande wa mashtaka, akionyesha uwezo wake wa kufuatilia kesi. Kwa msingi wa kuweka kumbukumbu, Mahakama pia iliona kwamba Mleta Maombi alipewa fursa ya kujitetea, ikiwa ni pamoja na kuwaita mashahidi, ingawa alichagua kutoa ushahidi yeye mwenyewe. Katika hali hiyo, Mahakama ilibaini kwamba haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki haikukiukwa.

Kuhusu fidia ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali madai ya uharibifu wa mali kutokana na kukosekana kwa uhusiano kati ya kisababishi cha uharibifu wa mali unaodaiwa kufanywa na ukiukaji wa haki zake za uhai, na utu kwa mujibu wa Vifungu vya 4, na 5 vya Mkataba vinavyounga mkono ushahidi. Kwa kutumia busara yake, ilitoa Sh. 300,000 kama fidia ya hasara ya maadili kwa Mleta Maombi. Madai ya hasara ya kimaadili kwa niaba ya wanufaika pia yalikataliwa kwa kushindwa kuthibitisha uhusiano wa kinasaba kati yao na Mleta Maombi.

Kuhusu fidia isiyo ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi ya kuondolewa kwenye jele ya wanaosubiri kifo, kwa kushindwa kuonyesha mazingira ya kipekee ya kulazimisha uamuzi huo kutolewa. Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi ya kesi yake kusikilizwa tena kuhusiana na hukumu yake kwa msingi kwamba uamuzi wa Mahakama kuhusu ukiukaji wa Mkataba haukuathiri hukumu yake. Aidha, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya kubadilisha hukumu ya Mleta Maombi kuwa kifungo cha maisha kwa msingi kwamba Mahakama hii si mamlaka ya mahakama ya rufaa na haisikilizi kesi zilizoamuliwa na mahakama za kitaifa.

Baada ya kubaini ukiukaji wa Vifungu vya 4 na 5 vya Mkataba kulingana na utoaji wa hukumu ya lazima ya kifo, kwa kunyongwa ili kurekebisha ukiukaji huu, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, bila kuchelewa, kuondoa kwenye sheria zake utoaji wa hukumu ya lazima ya kifo na kunyongwa kama njia ya kutekeleza

hukumu ya kifo. Pia, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi abatilishe hukumu hiyo, amwondoe Mleta Maombi kwenye adhabu ya kifo na asikilize tena kesi yao kuhusu hukumu kupitia utaratibu ambao unaruhusu busara ya mahakama. Aidha, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achapishe hukumu kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa na kuhakikisha kuwa hukumu hizo zinaendelea kupatikana kwa angalau mwaka mmoja tangu tarehe ya kuchapishwa.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28(7) cha Itifaki na Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya, Jaji Rafaâ Ben Achour an na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/042/2019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kupitia anwani ifuatayo ya barua pepe: registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*